

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SABA

KIKAO CHA TATU

31 OKTOBA, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SABA

KIKAO CHA TATU – TAREHE 31 OKTOBA, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 35 la tarehe 30 Agosti, 2024;
2. Toleo Na. 36 la tarehe 06 Septemba, 2024;
3. Toleo Na. 37 la tarehe 13 Septemba, 2024;
4. Toleo Na. 38 la tarehe 20 Septemba, 2024;
5. Toleo Na. 39 la tarehe 27 Septemba, 2024;
6. Toleo Na. 40 la tarehe 04 Oktoba, 2024;
7. Toleo Na. 41 la tarehe 11 Oktoba, 2024;
8. Toleo Na. 42 la tarehe 18 Oktoba, 2024; na
9. Toleo Na. 43 la tarehe 25 Oktoba, 2024;

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

38. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Stendi ya Kisasa Jiji la Arusha kupitia Mradi wa TACTIC.

39. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Afya Hunyari Bunda utakamilika.

WIZARA YA NISHATI:

40. MHESHIMIWA JESCA JONATHAN MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini ahadi ya Umeme jazilishi itatekelezwa kwenye Miji yenye sura za Vijiji kama Ugele, Mosi, Cargrielo, Machinjio, Ulonge, Mtalagala na Msisina.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

41. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMEDI KUHAUKA (LIWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itaweka Geti la kuingia Watalii kwenye Hifadhi ya Mwalimu Nyerere kwa upande wa Wilaya ya Liwale.

WIZARA YA KILIMO:

42. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahisha pembejeo na mbegu za ruzuku ya mahindi kabla ya kipindi cha masika Mbulu Vijijini.

43. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu kasi ndogo ya Mradi wa Umwagiliaji Kata ya Mwamkulu - Mpanda.

WIZARA YA UJENZI:

44. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Mkandarasi Mshauri wa Daraja la Malagarasi chini Kijiji cha Ilagala atamaliza kazi.

45. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini mradi wa ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kijiji cha Njianne - Kipatimu – Nandete hadi Nyamwage utaanza.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

46. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, lini Serikali itafanya mapitio na maboresho ya Sera ya Malezi ya Mwaka 1977 ikizingatiwa wakati huo hakukuwa na utandawazi kama ilivyo sasa.

WIZARA YA MADINI:

47. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini uzalishaji wa Madini ya NIOBIUM na Kiwanda cha Ferroniobium utaanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

V. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA
(LAAC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA
(PIC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
31 OKTOBA, 2024**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**